xii. Wasilisha ombi kwa kubofya palipoandikwa “Submit Application”

**ZINGATIA**

Nyaraka zinazohitajika wakati wa kuwasilisha maombi ya mabadiliko ya eneo la biashara ni:-

i. Uthibitisho wa eneo la Biashara; na
ii. Kibali kutoka Mamlaka za Udhibiti kwa biashara zinazo-dhibitiwa.

## 7. MAOMBI YA KUSITISHA MATUMIZI YA LESENI

Mabadiliko ya kusitisha matumizi ya Leseni ya biashara yana-fanywa pale biashara inapofungwa ikiwa bado na Leseni hai.

Baada ya kuingia kwenye mfumo fuata hatua zifuatazo:-:
Chagua huduma ya Leseni za Biashara (Business Licences);

i. Bofya palipoandikwa “Apply Now”;
ii. Chagua mahali palipoandikwa “Active Licence”;
iii. Chagua Leseni inayohitaji kufungwa;
iv. Bofya palipoandikwa “Action”
v. Chagua palipoandikwa “Cancellation”
vi. Jaza sababu za kusitisha matumizi ya Leseni husika;
vii. Hifadhi taarifa kwa kubofya palipoandikwa “Save”
viii. Wasilisha ombi “Submit Application”

## 8. JINSI YA KUOMBA AINA MPYA YA BIASHARA (NEW LINE OF BUSINESS TO AN EXISTING LICENCE)

Aina mpya ya biashara inaombwa kwenye eneo ambalo tayari lina leseni ya biashara iliyo hai; utaratibu huu unatumika endapo mfanyabiashara ameanzisha aina nyingine ya biashara kwenye eneo hilo hilo.

Baada ya kuingia kwenye mfumo, fuata hatua zifuatazo:-

i. Chagua huduma za leseni za biashara (business licences)
ii. Bofya palipoandikwa “Active Licence”
iii. Kwenye leseni ya biashara ya eneo husika bofya palipoandikwa “Action”
iv. Bofya palipoandikwa “Apply New Line of Business”
v. Thibitisha taarifa za eneo husika kwa bofya palipoandikwa “Declaration”
vi. Wasilisha ombi kwa kubofya palipoandikwa “Submit”

## 9. UTHIBITISHO WA KUTUMA MAOMBI

Baada ya kutuma ombi utapokea ujumbe kwenye barua pepe ukisema ombi lako limepokelewa na utapokea namba ya ufuatiliaji wa ombi husika.

## 10. KUANGALIA MCHAKATO WA MAOMBI UNAVYO ENDELEA

Mfumo umeweka uwazi wa mchakato wa ushughulikiaji wa maombi ambapo mwombaji anaweza kufuatilia mwenendo wa maombi yake kwa kuingia katika mfumo. Baada ya kuingia kwenye mfumo, fuata hatua zifuatazo:-

i. Bofya palipoandikwa “Submitted Application”.
ii. Hatua ambayo maombi yako yamefikia itaonekana kwenye jedwali la hali ya maombi (Status)

## 11. TAARIFA ZA MALIPO

Baada ya maombi ya Leseni ya biashara kupitishwa na kuidhinishwa, mwombaji utatumiwa barua-pepe ikiwa na ankara ya malipo ikiainisha kiasi cha malipo na namba ya malipo (Control Number) kwa ombi husika. Aidha, mwombaji anaweza kuingia na kuangalia taarifa za malipo katika mfumo kwa kufuata hatua zifuatazo:-

i. Bofya palipoandikwa “Submitted Application”
ii. Kisha Bofya palipoandikwa “Actions”
iii. kisha bofya palipoandikwa “View”
iv. kisha chagua palipoandikwa “Payment details”
v. Mwisho bofya “download invoice”

## 12. JINSI YA KUPATA LESENI

Baada ya kukamilika kwa malipo ya ada na ombi kuidhinishwa, mwombaji atapata Leseni husika katika mfumo na kuipakua. Baada ya kuingia katika mfumo fuata hatua zifuatazo:-

i. Bofya palipoandikwa “Active Licence”;
ii. Chagua Leseni husika;
iii. Bofya palipoandikwa “Action”
iv. Pakua leseni kwa kubwofya palipoandikwa “Download Licence”.

Kwa Taarifa zaidi

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY



# LESENI ZA BIASHARA KWA NJIA YA MTANDAO KUPITIA MFUMO ULIOBORESHWA WA UTOAJI LESENI BRELA Online Services (BOS)

## (MAELEKEZO KWA MUOMBAJI)

### LESENI ZA BIASHARA

Leseni ya Biashara kundi “A” ni kibali kinachotolewa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kwa mfanyabiashara kwa ajili ya kumruhusu kufanya biasha-ra yenye Sura ya kitaifa na kimataifa na zinazo ongozwa na sera katika ngazi ya Kitaifa au Kimataifa kwa mujibu wa Sheria ya Utoaji Leseni za Biashara (Sura 101). She-ria hiyo inamtaka kila mfanyabiashara kufanya biashara baada ya kuwa leseni ya biashara katika eneo ambapo biashara hiyo inafanyika.

### A. UTARATIBU WA KUPATA LESENI ZA BIASHARA KUNDI “A” KUTOKA BRELA

Maombi ya leseni za biashara kundi “A” yanafanywa na ku-wasilishwa BRELA kupitia Mfumo wa Utoaji huduma kwa njia ya Mtandao (BRELA Online Services Portal) kupitia tovuti https://bos.brela.go.tz. Ili kupata huduma-mtandao kwenye mfumo huu, ingia kwenye tovuti kwa kufuata hatua muhimu zifuatazo: -

## 1. KUJISAJILI KWENYE MFUMO

**A: KWA MTEJA MPYA**

i. Fungua Programu ya kuingia kwenye mtandao;
ii. Ingia kwenye tovuti https://bos.brela.go.tz;
iii. Bofya palipoandikwa *"Get Started";*
iv. Bofya palipoandikwa *"Create Account";*
v. Jaza taarifa zinazohitajika;
vi. Thibitisha usahihi wa taarifa;
vii. Gonga palipoandikwa *"Create Account"*
viii. Baada ya kugonga "Create Account, ujumbe utatumwa kwenye barua-pepe yako ukikutaka kuingia kwenye mfumo;

**B: MTEJA MWENYE AKAUNTI ORS**

i. Fungua programu ya kuingia kwenye mtandao;
ii. Ingia kwenye tovuti kupitia kiunganishi https://bos.brela.go.tz;
iii. Bofya palipoandikwa "Get Started";
iv. Bofya palipoandikwa "Forgot Password" kwa mwombaji ambaye ni kampuni au Jina la biashara;
v. Ingiza anwani ya barua pepe iliyosajiliwa kwenye ORS;
vi. Bofya palipoandikwa "Reset Password";
vii. Ujumbe utatumwa kwenye barua-pepe yako ukiwa na Namba za uthibitisho na kiunganisho cha kubadilisha nywila;
viii. Bofya kiunganisho ulichotumiwa na kuweka namba za uthibitisho;
ix. Ingiza nywila mpya na kuithibitisha;
x. Baada ya kuthibitisha nywila bofya palipoandikwa "Reset Password" na kuingia kwenye mfumo.\

## 2. JINSI YA KUINGIA KWENYE MFUMO WA BOS

i. Fungua programu ya kuingia kwenye mtandao;
ii. Ingia kwenye tovuti kupitia kiunganishi https://bos.brela.go.tz;
iii. Bofya palipoandikwa "Get Started";
iv. Bofya palipoandikwa "Login";
v. Ingiza barua pepe na nywila;
vi. Bofya palipoandikwa "Login";

## 3. JINSI YA KUOMBA LESENI MPYA YA BIASHARA

Baada ya kuingia kwenye mfumo, fuata hatua zifuatazo:-:

i. Chagua huduma ya Leseni za Biashara (Business Licences);
ii. Bofya palipoandikwa "Apply Now"
iii. Bofya palipoandikwa "New Business Licence"
iv. Bofya palipoandikwa "Apply New Licence".
v. Jaza taarifa zinazohitajika ambazo ni:-
   a. Taarifa kuhusu biashara inayoombewa Leseni;
   b. Taarifa za eneo la Biashara; na
   c. Taarifa za Mawasiliano.
vi. Hifadhi taarifa kwa kubofya palipoandikwa "Save"
vii. Ambatisha nyaraka zinazohitajika kwa kufuata maelekezo ya mfumo,
viii. Thibitisha taarifa na viambatisho kwa kubofya palipoandikwa "Declaration"
ix. Wasilisha ombi kwa kubofya palipoandikwa "Submit Application"

ZINGATIA: Nyaraka zinazotumika kama viambatisho kwa ombi jipya la leseni ya biashara ni:-

a. Uthibitisho wa eneo la Biashara;
b. Kibali kutoka Mamlaka za Udhibiti kwa biashara zinazodhibitiwa; na
c. Vitambulisho na Leseni za Makazi kwa wasio raia wa Tanzania.

## 4. JINSI YA KUHUISHA LESENI YA BIASHARA

Leseni inapaswa kuhuishwa ndani ya siku 21 tangu kuisha kwa muda wa matumizi wa Leseni husika.
Baada ya kuingia kwenye mfumo, fuata hatua zifuatazo:-:

i. Chagua huduma ya Leseni za Biashara (Business Licences);
ii. Bofya palipoandikwa "Apply Now"
iii. Bofya palipoandikwa "Expired Licence";
iv. Chagua Leseni husika;
v. Bofya palipoandikwa "Action";
vi. Bofya palipoandikwa "Renew";
vii. Bofya palipoandikwa "initialize Renew";
viii. Pitia na kuthibitisha taarifa za awali;
ix. Hifadhi taarifa kwa kubofya palipoandikwa "Save"
x. Ambatisha nyaraka zinazohitajika kwa kufuata maelekezo ya mfumo,
xi. Thibitisha taarifa na viambatisho kwa kubofya palipoandikwa "Declaration"
xii. Wasilisha ombi kwa kubofya palipoandikwa "Submit Application"

ZINGATIA: Nyaraka zinazohitajika wakati wa kuhuisha Leseni ni:-

i. Uthibitisho wa eneo la Biashara;
ii. Hati ya kutokudaiwa kodi;
iii. Kibali kutoka Mamlaka za Udhibiti kwa biashara zinazodhibitiwa; na
iv. Vitambulisho na Leseni za Makazi kwa wasio raia wa Tanzania.

## 5. JINSI YA KUOMBA LESENI YA TAWI

Leseni ya tawi inaombwa kwa biashara ambayo ina Leseni hai ya biashara katika ofisi kuu lakini inaanzisha biashara hiyo hiyo katika eneo jingine tofauti.

Baada ya kuingia kwenye mfumo, fuata hatua zifuatazo:-

i. Chagua huduma ya Leseni za Biashara (Business Licences);
ii. Bofya palipoandikwa "Apply Now"
iii. Chagua mahali palipoandikwa "Active Licence"
iv. Chagua Leseni kuu inayohitaji kuombewa Leseni ya Tawi
v. Bofya palipoandikwa "Action"
vi. Chagua palipoandikwa "Apply for Branch"
vii. Jaza taarifa za eneo lako la biashara "Business Location"
viii. Jaza taarifa za mawasiliano "Contact Information"
ix. Hifadhi taarifa kwa kubofya palipoandikwa "Save"
x. Ambatisha Nyaraka zinazohitajika kwa kufuata maelekezo ya mfumo;
xi. Thibitisha taarifa na viambatisho kwa kubofya palipoandikwa "Declaration"
xii. Wasilisha ombi kwa kubofya palipoandikwa "Submit Application"

**ZINGATIA:** Nyaraka zinazohitajika wakati wa kuomba Leseni ya tawi ni:-

i. Uthibitisho wa eneo la Biashara; na
ii. Kibali kutoka Mamlaka za Udhibiti kwa biashara zinazodhibitiwa.

## 6. MAOMBI YA KUFANYA MABADILIKO YA ENEO LA BIASHARA KWA LESENI ILIO HAI

Mabadiliko ya eneo la biashara yanaombwa kwa biashara ambayo ina Leseni hai lakini biashara hiyo inahamishwa kutoka eneo moja kwenda eneo jingine tofauti.
Baada ya kuingia kwenye mfumo, fuata hatua zifuatazo:-:

i. Chagua huduma ya Leseni za Biashara (Business Licences);
ii. Bofya palipoandikwa "Apply Now";
iii. Chagua mahali palipoandikwa "Active Licence";
iv. Chagua Leseni kuu inayohitaji kuombewa mabadiliko ya eneo la biashara;
v. Bofya palipoandikwa "Action"
vi. Chagua palipoandikwa "Apply for Change location"
vii. Jaza taarifa za eneo jipya la biashara
viii. Jaza taarifa za mawasiliano "Contact Information"
ix. Hifadhi taarifa kwa kubofya palipoandikwa "Save"
x. Ambatisha nyaraka zinazohitajika kwa kufuata maelekezo ya mfumo;
xi. Thibitisha taarifa na viambatisho kwa kubofya palipoandikwa "Declaration"